

MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA FEBRUARI, 2018 NA MWELEKEO WA MACHI, 2018

Dondoo za Machi, 2018

Taarifa hii inatoa muhtasari wa hali ya viashiria vya hali ya hewa na mwenendo wa mvua katika mwezi wa Februari, 2018 na mwelekeo wa viashiria na hali ya mvua kwa mwezi Machi, 2018 nchini.

- a) Mvua za *Masika* katika maeneo yanayozunguka Ukanda wa ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Mwanza, Geita, Mara, Shinyanga na Simiyu), Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro) na Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Dar es salaam na Pwani, maeneo ya kaskazini mwa mkoa wa Morogoro pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) zinatarajiwa kuanza katika wiki ya kwanza ya mwezi Machi, 2018.
- b) Mvua za '*Msimu*' katika maeneo yanayopata mvua mara moja kwa mwaka bado zinaendelea na mtawanyiko wake unatarajiwa kuwa wa kuridhisha.

1.0 MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA FEBRUARI, 2018 NA MATAZAMIO KWA MWEZI MACHI, 2018.

1.1 MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA FEBRUARI, 2018

Vipindi vya joto kali hususan katika maeneo ya mwambao wa pwani vimeripotwa katika mwezi Februari, hali hii imesababishwa na uwepo wa upepo wenye unyevu na joto kutoka ukanda wa Somalia kuelekea katika maeneo ya pwani ya nchi yetu.

2.0 MATAZAMIO MACHI, 2018

2.1 MIFUMO YA HALI YA HEWA

Joto la chini ya wastani linatarajiwa katika eneo la kati la Kitropikali la bahari ya Pasifiki pamoja na eneo la Pwani ya Angola, hata hivyo joto la juu ya wastani linatarajiwa katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi. Ukanda wa mvua (ITCZ), unatarajiwa kuanza kusogea kuelekea maeneo ya kaskazini mwa nchi yetu hivyo kupelekea kuanza kwa mvua kati ya wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Machi, 2018.

2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA MWEZI FEBRUARI, 2018

Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, maeneo ya kaskazini mwa mkoa wa Morogoro pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba): Vipindi kadhaa vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo hususan katika wiki ya kwanza ikifuatiwa na Ongezeko la mvua kuanzia wiki ya pili. Mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya kwanza ya mwezi Machi, 2018.

Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara): Ongezeko la mvua katika maeneo mengi linatarajiwa kuanzia wiki ya pili ya mwezi Machi. Mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya pili ya mwezi Machi, 2018.

Kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu): Vipindi kadhaa vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo, mvua zinatarajiwa kuanza kati ya wiki ya kwanza na ya tatu ya mwezi Machi, 2018.

Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): Vipindi vingi vya mvua vinatarajiwa hususan katika siku kumi za mwanzo za mwezi Machi, upungufu kidogo unatarajiwa kwa kipindi kilichosalia.

Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): Mvua zinatarajiwa kuongezeka hususan katika wiki mbili za mwanzo za mwezi machi, upungufu kidogo unatarajiwa kwa kipindi kilichosalia.

Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Njombe, Iringa, Mbeya pamoja na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro): Vipindi vingi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo mengi hususan wiki mbili za mwanzo wa mwezi machi, upungufu kidogo unatarajiwa kujitokeza kuanzia wiki ya tatu.

Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): Vipindi vya mvua vinatarajiwa hususan katika wiki mbili za mwanzo za mwezi machi, ikifuatiwa na upungufu wa mvua katika kipindi kilichosalia.

Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma): Vipindi vingi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo hususan katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Machi, ikifuatiwa na upungufu baada ya hapo.

Imetolewa na;

MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA